# MKATABA WA KUANZISHA, KUTEKELEZA NA KUGAWANA GHARAMA NA FAIDA ZA MRADI WA BIASHARA YA KABONI

KATI YA

**VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED (VCSL)**

NA

**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA KIHONDO,** NA
**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MAHARAKA,** NA
**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA, MISENGELE** NA
**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MSONGOZI,** NA
**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA SEWE KIPERA.**

## WILAYA YA MVOMERO, MKOA WA MOROGORO

**IMEANDALIWA NA:**


Mawalla Advocates
Mawalla Road Mawalla Heritage Park
Mawalla Law Offices, Plot No. 175/20
Arusha – Tanzania, P.O. Box 6101
Telefax: +255754282038 / +255 732 972 468
E-mail: info.arusha@mawalla.co.tz

**NA**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero
S.L.P 663,
**Mvomero**
Mkoa wa Morogoro

# Yaliyomo:

1.0. TAFSIRI NA MAANA ..... 4

2.0 MAWANDA YA MKATABA ..... 5

3.0 MADAI YA AWALI ..... 5

4.0 MISINGI YA JUMLA ..... 5

5.0 VIAMBATISHO VYA MKATABA ..... 6

6.0 MAJUKUMU YA WAHUSIKA WA MKATABA ..... 6

7.0 KAMATI MAALUM YA MRADI ..... 7

8.0 TAREHE YA KUANZA NA MUDA WA UTEKELEZAJI WA MKATABA ..... 8

9.0 UCHAKATAJI, UTHIBITISHAJI NA UUZAJI WA KREDIT ZA KABONI ..... 9

10.0 UTARATIBU WA MGAWANYO WA GHARAMA NA FAIDA ZA BIASHARA ..... 9

11.0 KUVUNJA MKATABA ..... 10

12.0 HALI ISIYOZUILIKA *(FORCE MAJEURE)* ..... 10

13.0 SHERIA ZITAKAZOTUMIKA ..... 11

14.0 USIRI WA MAWASILIANO NA KUTOA TAARIFA ..... 11

15.0 MASHARTI YA JUMLA ..... 11

16.0 VIAMBATISHO ..... 17

Mkataba huu wa kuanzisha, kutekeleza na kugawana gharama na faida za mradi wa biashara ya kaboni (utajulikana na kurejewa kama **"Mkataba"**), umefanyika leo siku ya **JUMATATU** tarehe **21.02.2025**; (na itajulikana na kurejewa kama **"Tarehe ya Kuanza"**),

KATI YA

**VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED,** kampuni binafsi yenye ukomo wa hisa iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura. 212 ya Sheria za Tanzania Toleo la 2020, yenye ofisi iliyosajiliwa iliyopo katika Ploti yenye Na. 245, Kitalu B – Msimbo wa Posta 14111, Mtaa wa Morocco / Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Kinondoni Dar es Salaam – Tanzania na yenye cheti cha usajili namba 157358928 (itajulikana kama VCSL au "**Mpendekezaji wa Mradi**") na pale ambapo muktadha utaruhusu, msemo huu utajumuisha wawakilishi wake wa kisheria, mawakala, wakabidhiwa na warithi wake katika cheo.

NA

Halmashauri ya Kijiji cha Kihondo, Kata ya Doma, chenye usajili Na. MOR-129-09003790, NA,
Halmashauri ya Kijiji cha Maharaka, Kata ya Doma, chenye usajili Na. MOR-129-09005869, NA,
Halmashauri ya Kijiji cha Misengele, Kata ya Doma, chenye usajili Na. MOR-129-09007322, NA,
Halmashauri ya Kijiji cha Msongozi, Kata ya Msongozi, usajili Na. MOR-129-09008219, NA,
Halmashauri ya Kijiji cha Sewe Kipera, Kata ya Doma, chenye usajili Na. MOR-129-09011293.

Halmashauri ya kijiji ni chombo cha kisheria kilichoanzishwa chini ya kifungu namba 22 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura. 287 ya Sheria za Tanzania, Toleo la 2002; (itajulikana kama **"Mmiliki wa Msitu").** Halmashauri ya kijiji ina anuani ya posta 663, Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro, Tanzania, na pale ambapo muktadha utaruhusu, itajumuisha Warithi, Wateule na Wakabidhiwa wake.

**AMBAPO**

A. Mmiliki wa Msitu ana nia ya kutumia Eneo la Mradi katika uendelezaji wa Miradi ya Kaboni ya misitu kupitia mfumo wa MKUHUMI.

B. Mpendekezaji wa Mradi amehiari kuingia katika mkataba baina yake na Mmiliki wa Msitu kwa ajili ya kushirikiana katika biashara ya kaboni.

C. Mmiliki wa Msitu na Mpendekezaji wa Mradi wanaridhia kuingia katika Mkataba kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Uendeshaji na Udhibiti wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022 na marekebisho yake ya mwaka 2023 ambao utachukua nafasi ya makubaliano yoyote ya awali kati Mmiliki wa Msitu na Mpendekezaji wa Mradi.

Kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyoainishwa hapa chini **INAKUBALIWA KAMA IFUATAVYO**:

## 1.0. TAFSIRI NA MAANA

1.1 **Andiko la Mradi** maana yake ni hati ya kina ya Mradi iliyothibitishwa na kuidhinishwa kwa mujibu wa kanuni, kwa kuzingatia viwango vya ubora na viwango vya kaboni, na kusajiliwa katika mifumo ya kitaifa na kimataifa ya biashara ya kaboni. Hati hii inaeleza mpango wa mradi wa kupunguza au kuzuia utoaji wa gesijoto zinazochangia mabadiliko ya tabianchi kwa kupunguza ukataji miti hovyo na uharibifu wa misitu katika Eneo la Mradi.

1.2 **Biashara** maana yake ni Biashara ya Kaboni, ambayo msingi wake ni mauzo ya krediti za kaboni kutokana na kupungua kwa ukataji miti hovyo na uharibifu wa msitu ulio katika Eneo la Mradi.

1.3 **Eneo la Mradi** linamaanisha misitu yote yenye umri usiyopungua miaka 10 kuanzia kipindi cha uthibitishaji wa kredit za kabon kwa mara ya kwanza kulingana na mkataba huu, na iliyo ndani ya mipaka ya Eneo la Mradi iliyoonyeshwa katika Viambatisho vilivyoainishwa kifungu cha tano (d) (5.0 (d)).

1.4 **Jumuiya** maana yake ni chombo cha pamoja kilichoundwa/kitakachoundwa kwa ajili ya kuwezesha usimamizi wa pamoja na kuunganisha vijiji/mtaa vinavyonufaika na biashara kaboni katika kuhifadhi mazingira na kuhakikisha faida inayopatikana kutokana na biashara ya kaboni inawafikia wanufaika husika.

1.5 **Kanuni** maana yake ni Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni), Kulingana na Gazeti la Serikali Nambari 636/637 ya 2022 ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mara kwa mara.

1.6 **Kiwango cha Ubora** kinamaanisha hali ya tabia nchi *(climate),* Jamii *(community)* na Bioanuwai *(biodiverity)* kulingana na viwango vya VERRA au viwango vingine linganifu.

1.7 **Kizio cha Mradi** kinamaanisha kiwango cha upunguaji wa uzalishaji wa hewa ukaa (Kredit za Kaboni) inayotokana na shughuli za mradi wa MKUHUMI katika eneo la mradi.

1.8 **Kredit za kaboni** maana yake ni kiasi cha tani moja ya hewa ukaa au gesijoto nyingine linganifu, kilichothibitishwa kadiri ya viwango vinavyotumika katika biashara ya kaboni.

1.9 **Makubaliano ya Awali m**aana yake ni barua ya ridhaa ambayo mmiliki alimpatia Mpendekezaji wa Mradi ambayo ilimwezesha kufanya usajili wa Mradi kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Udhibiti wakati wa kuanza shughuli za mradi.

1.10 **Mhusika au Upande** maana yake ni Village Climate Solutions Limited (VCSL), na Mmiliki wa Msitu kila mmoja anaporejewa peke yake na **Wahusika** au **Pande** wanaporejewa pamoja.

1.11 **MKUHUMI** maana yake ni Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ukaa inayotokana na ukataji miti hovyo na Uharibifu wa Misitu.

1.12 **Mmiliki wa msitu** maana yake ni mmiliki/wamiliki wa misitu na ardhi inayohusika katika Eneo la Mradi kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

1.13 **Mradi** unamaanisha Mradi wa MKUHUMI ulioanzishwa na Village Climate Solutions Limited (VCSL) na kusajiliwa na VERRA, au mamlaka inayofanana na VERRA pamoja na Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa.

1.14 **Mratibu wa kitaifa** maana yake ni kituo kilichoanzishwa chini ya kanuni za Uendeshaji na Udhibiti wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022 au kanuni nyingine linganifu kwa ajili ya usimamizi wa biashara ya Kaboni kitaifa.

1.15 **Mamlaka ya Serikali za Mitaa** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya, Mamlaka ya Mji Mdogo, Halmashauri ya Mji, Manispaa au jiji ambayo Eneo la Mradi linapatikana.

1.16 **Uhakikishaji** unamaanisha kuhusiana na Mradi, uhakikishaji wa Kupungua kwa uzalishaji wa Hewa ukaa kwa mujibu wa taratibu za Msingi za Kiwango cha Kaboni na Kiwango cha Ubora, na 'iliyohakikishwa' ina maana linganifu.

1.17 **Uthibitishaji** unamaanisha mchakato wa tathmini na uthibitishaji wa Mradi kwa mujibu wa viwango na taratibu za Msingi zinazohusika na biashara ya kaboni, na 'iliyothibitishwa' ina maana linganifu.

1.18 **Viwango vya Kaboni** inamaanisha Viwango Vya Kaboni vilivyothibitishwa (VER) na Verra au shirika linganifu.

1.19 **Wajibu wa Msingi** maana yake ni majukumu ya mhusika au wahusika wa mkataba kulingana na kifungu 6.0.

1.20 **Shughuli za Mradi** ni shughuli zote zinazolenga kupunguza ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa misitu, pamoja na usajili, tathmini, uchakataji, uthibitishaji, uuzaji, na malipo yanayohusiana na krediti za kaboni kama ilivyoainishwa katika Andiko la Mradi.

## 2.0 MAWANDA YA MKATABA

2.1 Mkataba huu ni kwa ajili ya uanzishaji na Utekelezaji wa Biashara ya Kaboni kupitia mfumo wa MKUHUMI Katika eneo la mradi. Ramani pamoja na taarifa zote muhimu za eneo la mradi zitakuwa kama zilivyoainishwa katika kifungu 5.0

2.2 Mkataba huu haubadilishi au kuathiri nafasi ambazo Wahusika wanazo, au ambazo wanaweza kuwa nazo, kuhusu mamlaka yao, wajibu au mamlaka yao ya kufanya maamuzi, wala hayatatafsiriwa kwa namna ambayo itaenda kinyume na mamlaka hiyo ya kufanya maamuzi kinyume na sheria isipokuwa kwa kuzingatia uwakilishi, ahadi, maagano au wajibu uliofanywa.

## 3.0 MADAI YA AWALI

**Mpendekezaji wa Mradi** amethibitisha hana madai yoyote kwa Mmiliki wa Msitu kutokana na shughuli za awali alizozitekeleza na ameridhia Makubaliano yoyote ya awali yaliyokuwepo yafike kikomo kwa nafasi yake kuchukuliwa na Mkataba.

## 4.0 MISINGI YA JUMLA

Katika utekelezaji wa Mkataba huu, pande zinazohusika zitazingatia misingi ifuatayo: -

a) Utunzaji endelevu wa mazingira
b) Maendeleo endelevu

c) Uwazi
d) Uwajibikaji
e) Utii wa sheria

## 5.0 VIAMBATISHO VYA MKATABA

Viambatisho vifuatavyo vitakuwa sehemu ya Mkataba huu:

a) Cheti cha Usajili wa Kampuni *(kiambatisho Na. 2)*
b) Cheti cha namba ya mlipakodi *(Kiambatisho Na. 3)*
c) Ramani ya Eneo la Mradi *(Kiambatisho Na. 1 (a))* na Ukubwa wa Eneo la Mradi *(Kiambatisho Na. 1 (b))*
d) Muhtasari wa Kikao cha Halmashauri ya Kijiji, Mkutano Mkuu wa Kijiji, na Mkutano wa baraza la Madiwani la Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyodhinisha Mmiliki wa Msitu kuingia katika Mkataba huu *(itarejewa kama kiambatisho Na. 4).*

## 6.0 MAJUKUMU YA WAHUSIKA WA MKATABA

Katika Mkataba huu pande zinazohusika zitakuwa na Majukumu kama ifuatavyo:

### 6.1 Majukumu ya Mpendekezaji wa Mradi

a) Kufanya usajili wa biashara ya kaboni;
b) Kuandaa andiko na kutekeleza mradi wa biashara ya kaboni;
c) Kushirikiana na Mmiliki wa Msitu na wadau wengine katika kuandaa na kutekeleza biashara ya kaboni kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi;
d) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa biashara ya kaboni kwa Mmiliki wa Msitu, na Mratibu wa kitaifa wa biashara ya kaboni kulingana na kanuni.
e) Kuwezesha Uhakiki na Uthibitishaji wa kredit za kaboni zinazotokana na shughuli za Mradi.
f) Kuchakata, kuhaulisha na kuuza krediti za kaboni zitazozalishwa katika eneo la mradi katika soko la hiari (*voluntary carbon market*) kwa mujibu wa sheria za soko husika kwa kipindi cha mkataba.
g) Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kutoa ushauri wa kitaalamu na mafunzo ya uendelezaji wa biashara ya Kaboni na mabadiliko ya tabianchi.
h) Kugawanya mapato ya kaboni kwa wadau wa mkataba kwa kuzingatia kanuni.
i) Kuwatambulisha watumishi watakaosimamia utekelezaji wa mradi kwa Mmiliki kadiri ya mahitaji.

### 6.2 Majukumu ya Mmiliki wa Msitu

a) Kusimamia utekelezaji wa mkataba huu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
b) Kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira katika maeneo yao.
c) Kutoa uthibitisho wa umiliki wa Eneo la Mradi linalohusika katika biashara ya kaboni kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.

d) Kufanya juhudi zote kuzuia ukataji miti ndani ya Eneo la Mradi na kuhakikisha uvunaji hautazidi 1% ya uzitohai wa miti iliyo katika Eneo la Mradi kwa mwaka kwa kuzingatia miongozo iliyoandaliwa na kukubalika kisheria, na mpango wa uvunaji endelevu ulioidhinishwa kisheria.

e) Kulinda, kutunza, kudhibiti na kusimamia Eneo la Mradi kulingana na masharti ya mkataba huu. Mipaka ya eneo la mradi haitabadilishwa bila ridhaa ya wahusika wote.

f) Kumpa haki Mpendekezaji wa Mradi ya kuchakata, kuhaulisha na kuuza krediti za kaboni zitokazozalishwa katika Eneo la mradi katika soko la hiari kwa mujibu wa sheria za soko hilo.

g) Kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha zinazotokana na biashara ya kaboni kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, kulingana na sheria, kanuni na taratibu za Tanzania.

h) Kushirikiana na Mpendekezaji wa Mradi na wadau wengine katika kuandaa na kutekeleza biashara ya kaboni kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi;

i) Kuandaa na kutekeleza kwa uthabiti mpango wa usimamizi wa msitu na sheria ndogo zinazohakikisha ulinzi na usimamizi endelevu wa Eneo la Mradi kwa muda wote wa mkataba huu.

j) Kutoa kwa mpendekeza mradi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, takwimu za maendeleo ya usimamizi wa msitu ulio katika Eneo la Mradi, matumizi ya fedha zinazotokana na mradi pamoja na hali ya maendeleo ya jamii angalau kila baada ya miezi mitatu au wakati wowote zitakapohitajika.

k) Kuandaa na kutekeleza Makubaliano ya Usimamizi wa Pamoja yanayowawezesha wanajamii katika mitaa (au kitongoji) kuwa Msimamizi wa misitu, na kupata mgawanyo wa gharama na faida kwa kiwango sawa na Mmiliki wa Msitu.

6.3 **Majukumu ya jumla**

a) Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za kupunguza ukataji miti hovyo na uharibifu wa misitu kwa lengo la uzalishaji wa hesabu za kredit za kaboni kwa kuzingatia viwango vya kaboni na viwango vya ubora katika Eneo la Mradi;

b) Kufanya shughuli zote za mradi kulingana na Sheria za Tanzania;

c) Kuhakikisha biashara ya kaboni inakuwa chachu ya kuimarisha uhifadhi na kukuza maendeleo ya jamii katika eneo la Mmiliki na Msimamizi

## 7.0 KAMATI MAALUM YA MRADI

7.1 Kulingana na mahitaji mahususi wakati wa utekelezaji, wahusika wanaweza kuunda kamati maalum ya mradi.

7.2 Wajumbe wa kamati watateuliwa kulingana na aina ya shughuli ya mradi itakayokuwa inafanyiwa kazi wakati husika. Wajumbe watakaoteuliwa wanaweza kujumuisha wajumbe wafuatao: -

i. Katibu Tawala Msaidizi anayeratibu sekta za Mazingira ngazi ya Mkoa;

ii. Afisa Mwandamizi anayeshughulikia usimamizi wa biashara ya Kaboni katika mamlaka ya serikali za mitaa husika.
iii. Mwanasheria wa Mamlaka ya serikali za mitaa
iv. Afisa Mipango wa Mamlaka ya serikali za mitaa;
v. Mhasibu wa Mamlaka ya serikali za mitaa;
vi. Mpendekezaji wa Mradi
vii. Mmiliki wa msitu
viii. Wajumbe waalikwa kutoka TRA, TIC na yeyote atakayehitajika kwa wakati huo

7.3 **Majukumu ya Kamati**

a) Kutoa ushauri wa kitaalamu, usimamizi na uzingatiaji wa matakwa ya kisheria katika utekelezaji wa shughuli za biashara ya kaboni katika eneo husika Pale itakapohitajika.
b) Kuandaa na kufanya uhakiki juu ya uzingatiaji wa Kanuni na Miongozo ya matumizi ya fedha zinazotokana na mradi katika Eneo la Mradi.
c) Kufuatilia chachu ya biashara katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa wananchi katika eneo husika kutokana na uwepo wa biashara ya kaboni.
d) Kufanya mapitio na marekebisho ya mkataba pale itakapohitajika.
e) Kufanya upatanishi pale ambapo kunatokea kutokuelewana baina ya wahusika.
f) Kutekeleza majukumu mengine kwa kadri ya mahitaji pasipo kuathiri matakwa ya Kanuni, Miongozo ya Biashara ya Kaboni na mkataba kati ya Mmiliki msitu na Mpendekezaji wa Mradi;

7.4 **Vikao vya kamati**

Kamati maalum ya mradi inaweza kutengeneza kanuni za vikao kuendana na majukumu yake.

7.5 **Gharama za Kamati**

Kila mjumbe au mshiriki wa kamati atalipiwa na taasisi anayotoka gharama za kutekeleza shughuli za kamati ikiwa na pamoja na posho za kujikimu, usafiri na gharama za kurudufu taarifa na nyaraka muhimu kulingana na taratibu za taasisi hiyo.

## 8.0 TAREHE YA KUANZA NA MUDA WA UTEKELEZAJI WA MKATABA

8.1 **Kuanza kwa Shughuli za Mradi:** Mpendekezaji wa Mradi alianza kushirikiana na Mamlaka za Usimamizi kutekeleza Shughuli za Mradi kuanzia tarehe 9, Februari 2023, kama ilivyoainishwa kwenye Andiko la Mradi.

8.2 **Kuanza kwa Mkataba:** Mkataba huu utaanza kutumika tangu Tarehe ya Kuanza, na utajumuisha krediti zote za kaboni zilizozalishwa au zitakazozalishwa tangu kuanza kwa shughuli za Mradi na kuthibitishwa baada ya Tarehe ya Kuanza.

8.3 **Muda wa Mkataba:** Mkataba huu utadumu kwa kipindi cha Miaka arobaini (40) au utakapositishwa kabla ya muda huo kwa mujibu wa mkataba, na utajumuisha shughuli

zote zilizofanyika au zitakazofanyika tangua kuanza kwa shughuli za Mradi, kama ilivyoainishwa katika Andiko la Mradi.

8.4 Wahusika wanaweza, kuongeza muda wa Mkataba huu kwa makubaliano ya maandishi.

8.5 **Mapitio na marekebisho ya Mkataba**

a) Mkataba huu unaweza kufanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitano (05) ndani ya kipindi chote cha utekelezaji, kadiri ya mahitaji, kwa lengo la kuboresha shughuli zinazolenga kupunguza ukataji miti hovyo, uharibifu wa misitu, na biashara ya kaboni, na marekebisho hayo yatakuwa sehemu ya mkataba huu baada ya Wahusika kukubaliana kwa maandishi na kusaini marekebisho hayo.

b) Endapo patatokea dharura itakayohitaji kufanya mapitio ya mkataba na kurekebisha baadhi ya vipengele vya mkataba huu, pande zote zinaweza kufanya hivyo kabla ya kufikia kipindi kilichotajwa katika kipengele cha 8.1(a), bila kuathiri masharti ya kipengele hicho.

## 9.0 UCHAKATAJI, UTHIBITISHAJI NA UUZAJI WA KREDIT ZA KABONI

9.1 Mmiliki wa Msitu amempa Mpendekezaji wa Mradi haki na wajibu wa kuchakata, kuthibitisha, kusajili, kuhaulisha, na kuuza krediti za kaboni zitakazozalishwa katika Eneo la Mradi kwenye soko la hiari *(voluntary carbon market)* kwa mujibu wa sheria za soko hilo kwa Kipindi chote cha Mradi, kitakachohesabiwa kuanzia tarehe 9 Februari 2023, kulingana na Andiko la Mradi.

9.2 Mpendekezaji wa Mradi atatumia Mbinu ya Viwango vya Kaboni (VCS) iliyoidhinishwa, na Viwango vya Ubora (CCB) katika kutathmini kiwango cha kupungua kwa uzalishaji wa gesi joto katika Eneo la Mradi na kuainisha kiasi cha kredit za kaboni ambazo zinaweza kusajiliwa na kuuzwa.

9.3 Mpendekezaji wa Mradi ataingia makubaliano na Shirika la Uthibitishaji na Uhakiki lililoidhinishwa na Viwango vya Kaboni na Viwango vya Ubora ili kuhakiki ripoti za ufuatiliaji na tathmini ya kredit za kaboni zitakazozalishwa katika Eneo la Mradi.

## 10.0 UTARATIBU WA MGAWANYO WA GHARAMA NA FAIDA ZA BIASHARA

Kwa madhumuni ya mkataba, pande zote zinakubaliana kuhusiana na mgawanyo wa gharama na faida kama ilivyoainishwa na kanuni:

a) Mmiliki wa Msitu atapata kiasi kisichopungua asilimia 51% ya mapato ghafi kutokana na mauzo ya viwango vya kaboni vilivyothibitishwa.

b) Mgawanyo wa gharama na faida kwa mamlaka za Usimamizi utazingatia vigezo viwili ambavyo ni kiwango cha kupunguza ukataji miti hovyo na uharibifu wa msitu, na kiasi cha kaboni kwenye Eneo la Mradi linalodhibitiwa na Mmiliki au Msimamizi.

c) Mamlaka ya serikali za mitaa itapata asilimia 8% ya mapato ghafi kulingana na kanuni.

d) Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itapata asilimia 2% ambapo asilimia 1% itabaki katika Wizara husika na asilimia 1% inayobaki itapelekwa katika

Sekretarieti ya mkoa kwa ajili ya kuwezesha uratibu wa utekelezaji wa biashara kulingana na kanuni pamoja na jitihada za uhifadhi wa mazingira.

e) Mpendekezaji wa Mradi atapata asilimia 31%ya mapato ghafi

f) Asilimia 8% iliyobaki italipwa kwa mamlaka ya Taifa ya uratibu au mratibu wa kitaifa.

g) Katika kutekeleza masharti katika vipengele (a) mpaka (d) hapo juu, Mpendekezaji wa Mradi atalipa mgao wa fedha kupitia akaunt au utaratibu ulioidhinishwa na chombo cha juu cha maamuzi cha taasisi husika, kwa kuzingatia kanuni na Sheria za Fedha za Tanzania.

## 11.0 KUVUNJA MKATABA

Endapo upande wowote utakiuka masharti ya mkataba isipokuwa kama imesababishwa na hali isiyozuilika (Force majeure), na kusababisha athari, mgogoro au tofauti yoyote kati ya wahusika wa mkataba huu, usuluhishi utafuata utaratibu ufuatao:

11.1 Wahusika watatumia mbinu za kidiplomasia kupata suluhu kama ifuatavyo:

a) Watajadiliana wenyewe namna ya kurekebisha dosari iliyojitokeza ndani ya muda watakaokubaliana.
b) Itakapobidi watatafuta Mpatanisi (mediator) ikiwa ni pamoja na Kamati maalum ya mradi, Mkuu wa mkoa, Mratibu wa Kitaifa, Wizara inayohusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa kama watakavyokubaliana.

11.2 Endapo mgogoro umeshindwa kutatuliwa na mpatanishi katika kipengele 11.1 ndani ya siku tisini (90), ikiwa ni pamoja na kushindwa kukubaliana juu ya Mpatanishi basi mgogoro huo utapelekwa kwa msuluhushi *(abitrator)* ambaye ana ujuzi wa kutosha/uliothibitishwa kwenye biashara na sheria za kaboni, kwa mujibu wa Sheria ya Uamuzi, Sura. 15 ya Sheria za Tanzania Toleo la 2020.

## 12.0 HALI ISIYOZUILIKA *(FORCE MAJEURE)*

12.1 Katika mkataba huu, hakuna upande utakaohusika kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake iwapo kushindwa huko ni kutokana na matokeo ya hali isiyozuilika kama vile;

a) majanga ya asili (mf; moto, mafuriko, tetemeko la ardhi, radi na dhoruba nk),
b) vitendo vya uadui wa umma (mf; vita, uvamizi, ugaidi, ghasia, machafuko, uasi, vizuizi mapinduzi nk),
c) Amri ya mamlaka halali (mf; kuwekwa chini ya ulinzi, kuzuiwa, katazo nk)
d) Sera na Sheria za nchi zitakazofanya Mpendekezaji wa Mradi asiwe na uwezo wa kuuza tena kredit za kaboni (mf; Ushuru usiolipika kibiashara, vikwazo nk).
e) Kusitishwa kwa shughuli za biashara ya kaboni. (mf; kukoma kwa soko la hiari la kimataifa au la kikanda, kukoma kwa shughuli za shirika la viwango vya kaboni nk).

12.2 Endapo Mpendekezaji wa mradi au Mmiliki wa Msitu atadai kuwa hali isiyozuilika *(Force majeure)* kama sababu ya kushindwa kutekeleza majukumu yake, atatakiwa kuthibitisha

hatua zinazostahili kuchukuliwa chini ya mazingira ya wakati husika ili kupunguza kuchelewa au uharibifu unaosababishwa na matukio yanayoonekana.

## 13.0 SHERIA ZITAKAZOTUMIKA

Mkataba huu utasimamiwa na sheria za Tanzania.

## 14.0 USIRI WA MAWASILIANO NA KUTOA TAARIFA

14.1 Katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu, mawasiliano yoyote yanayohusu mkataba huu yatafanyika kwa njia ya maandishi kwa kuzingatia usiri wa nyaraka na mawasiliano hayo kwa kutotoa taarifa zozote kwa mtu asiyehusika.

14.2 Mpendekezaji wa Mradi anaruhusiwa kukusanya taarifa zinazohitajika kwa ajili ya upembuzi, uandaaji wa taarifa za tathmini ya maendeleo ya mradi, na uchakataji wa kredit za kaboni katika eneo la mradi kulingana na mahitaji ya viwango vya kaboni na viwango vya ubora.

14.3 Mpendekezaji wa Mradi atashiriki katika mikutano rasmi ya Mmiliki na Msimamizi ili kujadili matokeo ya Mradi, Kutoa wasilisho la kina la vipimo vya utendaji wa Mradi, uzalishaji wa kredit za kaboni, na mbinu iliyotumika kukokotoa malipo ili kuhakikisha uwazi wa kifedha, miongoni mwa mengine.

**14.4** Anuani za mawasiliano zitakazotumika zimetolewa hapa chini:

**Kwa Mpendekezaji wa Mradi:**

Kwa: Mkurugenzi
Village Climate Solutions Limited
Ali Hassan Mwinyi, Nambari ya Ploti 245
Nambari ya Kitalu B, Nambari ya Nyumba 245
Dar es Salaam - Tanzania

**Kwa Mmiliki:**

Kwa: Afisa Mtendaji wa Kijiji
S.L.P 663
**MVOMERO**

## 15.0 MASHARTI YA JUMLA

### 15.1 Matumizi ya eneo la mradi

Wahusika hawataingia kwenye makubaliano au mikataba mingine au kutekeleza shughuli zinazokinzana na mkataba huu.

### 15.2 Uhalali

Mkataba huu utakuwa halali katika kipindi chote cha utekelezaji, endapo kutakuwa mabadiliko ya kisheria, kanuni, taratibu na miongozo ya biashara ya kaboni pamoja na masharti ya mkataba, wahusika watafanya marekebisho ya vipengele vilivyoathiriwa na mabadiliko hayo.

### 15.3 Kustahimili

Kuvunjika kwa Mkataba huu hakutaathiri haki au wajibu wowote ambao unaweza kuwa ulipatikana kabla ya kuvunjika, ikijumuisha haki au wajibu wowote kuhusiana na ukiukaji uliotangulia, ikiwemo wajibu wa kulipa kodi na kutii sheria za nchi.

### 15.4 Mkataba mzima

Mkataba mzima ni kwa ajili ya kuanzisha, kutekeleza na kugawana gharama na faida za biashara ya kaboni. Mkataba huu unachukua nafasi ya makubaliano, maelewano, au uwakilishi wa awali kuhusiana na biashara ya kaboni kati ya wahusika

**KWA USHUHUDA HUU**, Wahusika hapa wamesaini Mkataba huu wa uanzishaji na Utekelezaji wa mradi wa biashara ya kaboni na ugawanaji wa gharama na faida tangu kuanza kwa shughuli za mradi.

Watu wafuatao wameidhinishwa na Halmashauri ya Kijiji cha **Kihondo** kuweka sahihi Mkataba huu kwa ajili na kwa niaba ya **Mmiliki wa Msitu.**

Jina: YUSTA ALFANI SELEMANI

Cheo: Mwenyekiti wa Kijiji

Sahihi:

Tarehe: 03.03.2025

Jina: WILNELY YUSTINI SELEMANI

Cheo: Afisa Mtendaji wa Kijiji

Sahihi: AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA KIHONDO P.O. 663 - MVOMERO

Tarehe: 03.03.2025

Watu wafuatao wameidhinishwa na Halmashauri ya Kijiji cha **Maharaka** kuweka sahihi Mkataba huu kwa ajili na kwa niaba ya **Mmiliki wa Msitu.**

Jina: COSTA A MSIMANGE

Cheo: Mwenyekiti wa Kijiji

Sahihi: Amsimange

Tarehe: 3.3.2025

Jina: ELIZA ELENEUS MCHILO

Cheo: Afisa Mtendaji wa Kijiji

Sahihi: Mchilo AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA MAHARAKA

Tarehe: 03.03.2025

---

Watu wafuatao wameidhinishwa na Halmashauri ya Kijiji cha **Misengele** kuweka sahihi Mkataba huu kwa ajili na kwa niaba ya **Mmiliki wa Msitu.**

---

Jina: LAMECKI Y MANGELE

Cheo: Mwenyekiti wa Kijiji

Sahihi: MWENYEKITI WA SERIKALI YA KIJIJI CHA MISENGELE

Tarehe: 3/3/2025

Jina: CHOLETA J. NGAVUMBA

Cheo: Afisa Mtendaji wa Kijiji

Sahihi: Ngavumba AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA MISENGELE

Tarehe: 03/03/2025

---

Watu wafuatao wameidhinishwa na Halmashauri ya Kijiji cha **Msongozi** kuweka sahihi Mkataba huu kwa ajili na kwa niaba ya **Mmiliki wa Msitu.**

---

Jina: SALEHE SALUMU SAIDI

Cheo: Mwenyekiti wa Kijiji

Sahihi:

Tarehe: 03/03/2025

Jina: ZAINABU LEONARD JOHN

Cheo: Afisa Mtendaji wa Kijiji

Sahihi: AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHA MSONGOZI

Tarehe: 03/03/2025

---

Watu wafuatao wameidhinishwa na Halmashauri ya Kijiji cha **Sewe Kipera** kuweka sahihi Mkataba huu kwa ajili na kwa niaba ya **Mmiliki wa Msitu.**

---

Jina: MOHAMEDI IDDI LUGOD

Cheo: Mwenyekiti wa Kijiji

Sahihi:

Tarehe: 03-03-2025

HALMASHAULI YA KIJIJI CHA SEWE KIPERA P.O.BOX 663 MVOMERO

Jina: ALLY YUSUPH KSABEJUP

Cheo: Afisa Mtendaji wa Kijiji

Sahihi:

Tarehe: 03-03-2025

AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA SEWE KIPERA P.O.BOX 663 MVOMERO

Watu wafuatao wameidhinishwa na **Village Climate Solutions Limited** kuweka sahihi Mkataba huu kwa ajili na kwa niaba ya **Mpendekezaji wa Mradi.**

Jina: CHARLES MESHACK

Cheo: DIRECTOR

Sahihi:

Tarehe: 25/03/2025

VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED
PLOT 40 - BLOCK Z - WAILES
LINDI - TANZANIA

Jina: EMMANUEL WILLIAM WALALA

Cheo: DIRECTOR

Sahihi:

Tarehe: 25/03/2025

**Uthibitisho wa Mwanasheria: Imetiwa Muhuri na kutolewa kwa Lakiri Mbele yangu leo tarehe:**

Jina: THERESIA. K. MAWALLA

Cheo ADVOCATE

Sahihi

Tarehe 25/03/2025

**Uthibitisho wa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Mvomero: Imetiwa Muhuri na kutolewa kwa Lakiri Mbele yangu leo tarehe**

Jina: LOEMA PETER ISAAY

Cheo Mkurugenzi Mtendaji Wilaya

Sahihi

Tarehe 07/03/2025

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA (W) MVOMERO
S.L.P 663, MOROGORO

**Uthibitisho wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero: Imetiwa Muhuri na kutolewa kwa Lakiri Mbele yangu leo tarehe:**

Jina: YUSUPH AHMADI MAKUNGA

Cheo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero

Sahihi 25/3/2025

**Uthibitisho wa Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero: Imetiwa Muhuri na kutolewa kwa Lakiri Mbele yangu leo tarehe:**

Jina: SERAPHINA VENAS RUFUNDI

Cheo Mwanasheria wa Wilaya ya Mvomero

Sahihi 25/3/2025


MVOMERO DISTRICT COUNCIL
DISTRICT LEGAL OFFICER
P.O. Box 663
MOROGORO

## 16.0 VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1 (a):** ukubwa wa Eneo la Mradi – Kulingana na kifungu namba 5 (d) cha Mkataba

| | | Eneo la Msitu wa Kijiji | | Eneo la Mradi | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Namba** | **Mmiliki** | **Ukubwa (hekta)** | **Jumla (hekta)** | **Ukubwa (hekta)** | **Jumla (hekta)** |
| 156 | Kihondo | 2,208.07 | 2,208.07 | 2,003.69 | 2,003.69 |
| 758 | Maharaka | 446.62 | | 185.56 | |
| 759 | Maharaka | 4,714.02 | 5,160.64 | 3,370.56 | 3,556.12 |
| 748 | Misengele | 57.14 | | 54.06 | |
| 749 | Misengele | 4,540.26 | | 4,447.44 | |
| 750 | Misengele | 471.46 | 5,524.80 | 467.44 | 5,287.13 |
| 731 | Msongozi | 455.94 | | 318.19 | |
| 735 | Msongozi | 1,578.57 | | 822.63 | |
| 736 | Msongozi | 2,937.17 | 4,971.68 | 2,580.69 | 3,721.51 |
| 146 | Sewe Kipera | 9,097.01 | | 8,912.88 | |
| 720 | Sewe Kipera | 85.79 | | 85.63 | |
| 724 | Sewe Kipera | 28.58 | 9,211.38 | 28.13 | 9,026.64 |
| **Jumla** | | **26,620.63** | **27,076.57** | **23,276.90** | **23,595.09** |

**Kiambatisho Na. 1 (b):** Ramani ya Eneo la Mradi – Kulingana na kifungu namba 5 (d) cha Mkataba




**Kiambatisho Na. 2:** Cheti cha Usajili wa Kampuni - Kulingana na kifungu namba 5 (a) cha Mkataba

C.1

TANZANIA

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# Certificate of Incorporation of a Company

Section 15

## No: 157358928

I HEREBY CERTIFY THAT

## VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED

is this day incorporated under the Companies Act, 2002
and that the Company is Limited.

**GIVEN** under my hand at Dar es Salaam this **14th** day of
**AUGUST TWO THOUSAND AND TWENTY TWO**.

REGISTRAR OF COMPANIES ★ TANZANIA ★

*PRINC ASST. REGISTRAR OF COMPANIES*

**Kiambatisho Na. 3:** Cheti cha namba ya mlipakodi - Kulingana na kifungu namba 5 (b) cha Mkataba

CTIN: 613976

# TANZANIA REVENUE AUTHORITY

## CERTIFICATE OF REGISTRATION

## FOR

## TAXPAYER IDENTIFICATION NUMBER (TIN)

(ISSUED UNDER SECTION 23 OF THE TAX ADMINISTRATION ACT 2015)

## THIS IS TO CERTIFY THAT

**VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED**

HAS BEEN REGISTERED WITH THE TANZANIA REVENUE AUTHORITY AND ASSIGNED THE TAXPAYER IDENTIFICATION NUMBER

**157-358-928**

WITH EFFECT FROM: **14 August 2022**

TRA LOCATION: **LINDI** TAX OFFICE: **LINDI**

PHYSICAL LOCATION: **PLOT No. 40** **BLOCK No. Z**

**STREET / AREA: WAILES**

ELIJAH G. MWANDUMBYA

**OFFICIAL SEAL** **COMMISSIONER FOR DOMESTIC REVENUE**

NOTE: THE REQUIREMENTS UNDER WHICH THIS CERTIFICATE IS ISSUED ARE STATED OVERLEAF